



22140198



SWAHILI A: LITERATURE – HIGHER LEVEL – PAPER 2
SWAHILI A : LITTÉRATURE – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2
SWAHILI A: LITERATURA – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2

Monday 12 May 2014 (afternoon)

Lundi 12 mai 2014 (après-midi)

Lunes 12 de mayo de 2014 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied and compare and contrast these works in response to the question. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.
- The maximum mark for this examination paper is *[25 marks]*.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. En basant votre réponse sur au moins deux des œuvres de la troisième partie que vous avez étudiées, vous devez comparer et opposer ces œuvres dans le cadre du sujet. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la troisième partie n'obtiendront pas une note élevée.
- Vous n'êtes pas autorisé(e) à apporter des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d'examen.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est *[25 points]*.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Conteste una sola pregunta de redacción. Base su respuesta en al menos dos de las obras estudiadas de la Parte 3, comparándolas y contrastándolas en relación con la pregunta. Las respuestas que no se basen en al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán una puntuación alta.
- No está permitido traer copias de las obras estudiadas a la sala de examen.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[25 puntos]*.

Jibu swali moja tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi za sehemu ya 3 ulizojifunza na ulinganishe kazi hizi kuabatana na swali. Majibu ambayo hayatahusisha mjadala wa kazi za sehemu ya 3 hayatatunzwa alama za juu.

Tamthilia

1. Onyesha vile wahusika wa kazi za tamthilia wanavyotumika au kutotumika kama kioo cha kuangazia maswala tofauti ya kijamii kwa kuzingatia kazi mbili za waandishi wawili tofauti ulizozisoma.
2. Tofauti za kijinsia na za kiumri huathiri ukuzaji wa maudhui. Kwa kuzingatia kazi mbili za waandishi wawili ulizozisoma onyesha jinsi mwandishi anavyoonyesha ulinganifu wa kijinsia au kiumri ili kukuza mada yake.
3. Mazungumzo ni mbinu muhimu katika kuendeleza ploti ya mwandishi. Jadili kauli hii ukizingatia kazi mbili za waandishi tofauti ulizozisoma na uonyeshe jinsi wanavyofaulu au kutofaulu katika kukuza mbinu hii.

Riwaya

4. Jinsi mwandishi anavyotanguliza kazi yake humfanya msomi kuwa na fununu kuhusu ploti ya mwandishi. Thibitisha ukweli wa kauli hii ukitumia kazi mbili tofauti kutoka kwa waandishi wawili tofauti.
5. Mara nyingi msuko wa vitushi huchangia pakubwa katika kuleta ladha kwenye kazi za fasihi kuliko mtindo wa lugha anaotumia mwandishi. Jadili ukizingatia angalau kazi mbili za waandishi tofauti ulizozisoma.
6. Kwa kuzingatia kazi mbili kutoka kwa wasanii wawili tofauti ulizojitayarishia, jadili jinsi wahusika wanavyojisaka na kujitafuta kwa kujifahamu au kutojifahamu. Mwandishi amefaulu kiviipi kuwakuza wahusika wake katika nadharia hizi mbili.

Ushairi

7. Ushairi huibuka kutokana na tajriba, matukio na matarajiwa ya mwandishi. Huku ukizingatia wanashairi wawili kutoka kwa kazi mbili tofauti ulizojitayarishia, jadili jinsi maswala haya ya tajriba, matukio na matarajiwa yanavyowasilishwa na maandishi hawa.
8. Shairi huwa ni msuko wa mbinu nyingi za lugha zinazolifanya shairi kuwa kamilifu. Ni kwa kiasi gani wanashairi wa kazi mbili ulizojitayarishia wanavyofaulu kuunganisha mbinu hizi tofauti ili kufanikisha kazi zao.
9. Ushairi hujikita kwenye mazingira tofauti ya kijamii. Onyesha jinsi washairi wanavyotumia mazingira haya tofauti ili kuibua na kutatua matatizo haya ukizingatia kazi mbili za wanashairi wawili ulizojitayarishia.

Riwaya ya Mapenzi

10. Mapenzi huchukua mikondo na taswira tofauti. Onyesha mikondo na taswira tofauti inayochukuliwa na maandishi wa kazi mbili ulizojitayarishia na uonyeshe udhaifu na uthabiti wake.
 11. Onyesha vile maandishi wa kazi mbili kutoka kwa maandishi wawili tofauti wanavyotumia ploti ya kazi zao na ujadili jinsi inavyoathiri kukia kilele cha kazi zao.
 12. Maneno yanayotamkwa katika uhusiano wa wapendanao huleta ukinzano au uelewano wa kihisia. Jadili kauli hii huku ukionyesha jinsi matumizi ya lugha ya kimapenzi yanavyoathiriwa na matumizi tofauti ya maneno haya.
-